

Ukweli juu ya hadithi za uwongo, habari potofu na habari za kughushi zinazohusiana na COVID-19



Hadi leo, hakuna dawa maalum ambazo zimetambuliwa ambazo zinazuia au kutibu ugonjwa wa virusi vya corona (COVID-19).

Watu walioambukizwa wanapaswa kupata utunzaji sahihi wa kupunguza na kutibu dalili. Watu wanaougua au kuumwa sana wanapaswa kupatiwa huduma inayofaa. Matibabu fulani maalum yanachunguzwa, na yatatimwa kupitia majaribio ya kliniki.



Chloroquine sio tiba ya ugonjwa wa virusi vya corona (COVID-19).

Chloroquine inatumika kutibu ugonjwa wa malaria, na inafanyiwa majaribio kama tiba ya ugonjwa wa virusi vya corona (COVID-19). Lakini sio tiba, na majaribio yanaendelea. Kuwa mwangalifu: ingawa chloroquine kwa ujumla ni dawa salama, kumekuwa na baadhi ya kesi zilizoripotiwa za athari hasi za chloroquine.



Kuna uvumi wa uwongo kwamba "Damu ya Kiafrika na ngozi nyeusi inapingana na COVID-19."

Hakuna ushahidi wa kisayansi kuunga mkono hoja hii. Na Waafrika wengi ni kati ya wale walioambukizwa COVID-19.



Hauwezi kupata ugonjwa wa virusi vya corona (COVID-19) kwa kugusana na wanyama.

Kuna uvumi unaozunguka kwamba kuku na mifugo mingine inaweza kuambukiza binadamu ugonjwa wa virusi vya corona (COVID-19). Uvumi huu ni wa uwongo. Hakuna ushahidi wa kupendekeza kwamba mnyama wa aina yoyote anaweza kuambukiza binadamu ugonjwa wa virusi vya corona (COVID-19). Maambukizi ya binadamu husababishwa na muingiliano kati ya mtu na mtu au kugusana nyuso za vitu vyenye matone yenye virusi.



Kunywa pombe HAKUKUKINGI dhidi ya ugonjwa wa virusi vya corona (COVID-19) na inaweza kuwa hatari.

Kunywa pombe SIO KINGA dhidi ya COVID-19 na inaweza kuwa hatari. Pombe pekee ambayo Shirika la Afya Duniani linapendekeza kutumia kukabiliana na COVID-19 ni vitakatisha mikono vyenye pombe/kilevi. Kwa kweli, kunywa pombe mara kwa mara au kupita kiasi kunaweza kuongeza hatari kwako kwa kupata shida za kiafya kama saratani na uharibifu wa ini.



Chanjo inaweza kuwa tayari katika miezi michache.

Huu ni uwongo. Haiwezekani kwamba kutakuwa na chanjo kwa angalau mwaka



Dawa za kuuu bakteria HAZINA ufanisi katika kuzuia na kutibu ugonjwa wa virusi vya corona (COVID-19).

Dawa za kuuu bakteria hazifanyi kazi dhidi ya virusi, ni kwa bakteria tu. COVID-19 ni virusi na dawa za kuuu bakteria hazipaswi kutumiwa kuzuia au kutibu ugonjwa wa virusi vya corona (COVID-19). Walakini, ikiwa umelazwa hospitalini kwasababu ya COVID-19, unaweza kupokea dawa za kuuu bakteria kwa ajili ya kutibu maambukizo mengine




Kuna uvumi wa uwongo kwamba vitu vingine vinaweza kuponya au kuzuia maambukizi ya ugonjwa wa virusi vya corona (COVID-19).

Hii ni pamoja na kunywa mchanganyiko wa limao na baking soda, kuvuta mvuke kutoka katika maganda ya machungwa au malimao yaliyochemshwa, kula vyakula vyenye alkali, na kusukutua maji ya chumvi au maji ya ndimu. Kulingana na Shirika la Afya Ulimwenguni, njia ya kuzuia kutokuambukizwa ugonjwa wa virusi vya corona (COVID-19) na kuzuia virusi kusambaa, ni kuosha mikono yako mara kwa mara, kudumisha angalau umbali wa mita moja kati yako na mtu anayepiga chafya au kukohoa, epuka kugusa uso wako, na funika mdomo wako na pua na kiwiko chako cha mkono au tishu wakati unapokohoa au kupiga chafya



Kuota jua au kukaa kwenya joto zaidi ya nyuzi joto 25 HAKUZUI ugonjwa wa wa virusi vya corona (COVID-19).

Unaweza kupata ugonjwa wa virusi vya corona (COVID-19) bila kujali hali ya jua au joto ilivyo. Nchi zilizo na hali ya hewa ya joto zimeripoti visa vingi vya maambukizi ya ugonjwa wa virusi vya corona (COVID-19). Ili kujikinga, hakikisha unasafisha mikono yako mara kwa mara na epuka kugusa macho yako, mdomo na pua.



Kuna uvumi wa uwongo kwamba "kufanya ngono mara kwa mara huua virusi vya ugonjwa wa corona (COVID-19)"

Kama aina zingine za migusano, ufanyaji ngono unaweza kusababisha hatari ya kuambukizwa.



Kuoga maji ya moto au kutumia kikausha mikono cha joto HAITAKUKINGA wewe kupata maambukizi ya ugonjwa wa wa virusi vya corona (COVID-19).

Kulingana na shirika la Afya Ulimwenguni, tiba zingine zinaweza kusaidia kupunguza dalili za ugonjwa wa virusi vya corona (COVID-19), lakini hakuna ushahidi kwamba dawa yoyote iliyopo sasa au shughuli yoyote inaweza kuzuia au kuponya ugonjwa huo.



Kula vitunguu swaumu HAKUWEZI kusaidia kuzuia maambukizi ya ugonjwa wa virusi vya corona (COVID-19).

Vitunguu swaumu ni chakula cha afya ambacho kinaweza kuwa na viua bakteria. Walakini, hakuna ushahidi kwamba kula vitunguu swaumu kunaweza kuwalinda watu dhidi ya ugonjwa wa virusi vya corona (COVID-19).



Ugonjwa wa virusi vya corona (COVID-19) hauwezi kuambukizwa kupitia kuumwa kwa Mbu.

Hakuna ushahidi kwamba COVID-19 inaweza kuambukizwa na mbu. COVID-19 huenea kupitia matone yanayotokana wakati mtu aliyeambukizwa anakohoa au kupiga chafya, au kupitia matone ya mate au kutoka kwenye pua.



Mawasiliano ya simu kiwango cha 5G HAYASAMBAZI ugonjwa wa virusi vya corona (COVID-19).

Virusi haviwezi kusafiri kwenye mawimbi ya redio au mitandao ya simu. COVID-19 inaenea katika nchi nyingi ambazo hazina mitandao ya simu ya mawimbi yenye kiwango cha 5G.



Kuwa na uwezo wa kushikilia pumzi yako kwa sekunde 10 au zaidi bila kukohoa au kujihisi vibaya HAINA maana huwezi kuwa na ugonjwa wa virusi vya corona (COVID-19).

Shirika la Afya Ulimwenguni linawashauri watu ambao wanafikiria wanaweza kuwa na ugonjwa wa virusi vya corona (COVID-19) kukaa nyumbani na kutafuta matibabu kwa kupiga simu mamlaka zao za kiafya. Njia bora ya kudhibitisha ikiwa unavyo virusi vya COVID-19 ni vipimo vya maabara. Hauwezi kujipima kwa zoezi hili la kupumua, ambalo linaweza kuwa hatari.